



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA MAFIA**



**Mafia  
28 Juni, 2024**


**TAARIFA KWA UMMA  
MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA SHILINGI BILIONI 1.04 (1,047,996,916.6)  
KWA AJILI YA UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU ELIMU YA AWALI NA MSINGI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia **Ndugu MUSSA A. KITUNGI** anapenda kuutaarifu Umma kuwa, Halmashauri imepokea fedha kiasi cha Shilingi 953,100,000 kutoka Serikali Kuu kupitia program ya BOOST kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya shule na Shilingi 94,896,916.60 kupitia program Endelevu ya Usambazaji wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (SRWSS) kama ifuatavyo:-

1. Fedha za ujenzi wa shule mpya ya msingi ya mkondo mmoja pamoja na nyumba ya walimu katika kijiji cha Kifinge Milioni, 404.9.
2. Fedha za ujenzi wa madarasa manne na matundu sita ya vyoo Shule ya Msingi Kilimahewa, Milioni 111.8.
3. Fedha za ujenzi wa madarasa manne na choo kimoja Shule ya Msingi Kungwi, Milioni 90.8.
4. Fedha za ujenzi wa madarasa manne Shule ya Msingi Dongo, Milioni 89.
5. Fedha za ukarabati wa Shule ya Msingi Utende, Milioni 101.
6. Fedha za ujenzi wa madarasa matatu na matundu sita ya vyoo Shule ya Msingi Chole, Milioni 77.8.
7. Fedha za ujenzi wa madarasa matatu na matundu sita ya vyoo shule ya Msingi Marimbani, Milioni 77.8.
8. Fedha za ujenzi wa matundu 11 ya vyoo pamoja na usambazaji wa maji Shule ya Msingi Ndagoni, Milioni 32.9
9. Fedha za ujenzi wa matundu 10 ya vyoo pamoja na usambazaji wa maji Shule ya Msingi Chunguruma, Milioni 30.9
10. Fedha za ujenzi wa matundu 10 ya vyoo pamoja na usambazaji wa maji Shule ya Msingi Chemchem, Milioni 30.9

Mkurugenzi Mtendaji kwa niaba ya Uongozi wa Wilaya ya Mafia, anatoa shukrani kwa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutoa fedha nyingi za Miradi ya maendeleo ambayo imeimarisha na kuboresha miundombinu mbalimbali.

Imetolewa na:



Emilian Mgumba  
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Halmashauri ya Wilaya ya Mafia.